

**IN THE HIGH COURT OF ZANZIBAR**  
HOLDEN AT VUGA  
MATRIMONIAL CIVIL CASE NO. 05 OF 2012

KATARINA KUWAKA

-----

PETITIONER

***VERSUS.***

JACKSON MABENGO

-----

RESPONDENT.

**H U K U M U.**

Rabia H. Mohamed, J.

Muombaji ***KATARINA KUWAKA*** na Muombewa ***JACKSON MABENGO*** ni mke na mume kwa ndoa iliyofungwa katika Kanisa Katoliki Pande (Kanda Kuu) huko Tanga tarehe 01 Septemba, 1996. Cheti cha Ndoa hiyo kilitolewa na kupokelewa Mahkamani kama Kielelezo P1.

Muombaji na Muombewa wamejaaliwa kupata watoto watano ambao wanne kati ya wapo hai. Watoto hao ni John Congress Mabengo (miaka 18), Joyce Congress Mabengo (miaka 16), Emmanuel Congress Mabengo (miaka sita na nusu) na Stephen Congress Mabengo (miaka mine).

Katika ndoa yao Muombaji na Muombewa walifanikiwa kununua banda ambalo baadae waliliendeleza kwa ujenzi wa nyumba ya kisasa. Nyumba hii imepakana upande wa Kaskazini ni Nyumba ya Rabia John, Kusini Nyumba ya Moh'd

Masoud, Mashariki Nyumba ya Tunza Ali na Magharibi Nyumba ya Issa Ramadhani.

Kuanzia mwaka 2006 maelewano katika ndoa ya Muombaji na Muombewa yalianza kupotea na mwisho kufikia hatua ya kila mmoja kushindwa kabisa kuishi na mwenziwe. Hivyo Muombaji amefungua shauri hili Mahkamani akiomba Mahkama kutengua ndoa yake na Muombewa na kumpatia talaka. Pia ameiomba Mahkama nyumba na vitu vyote vilivyomo ndani ambavyo alivitaja kuwa ni Kabati, friji kubwa na dogo, Baskeli mbili, Makochi ya kawaida na Sofa, Meza tatu kubwa, Viti vine, Stuli nne, "Television" moja, Radio mbili kubwa, Radio ndogo moja, Deki tatu, Cherehani moja. "Generator" moja, "Dish" moja, viuzwe na pesa itakayopatikana igaiwe nusu kwa nusu baina ya Muombaji na Muombewa. Muombaji pia ameiomba Mahkama kumpatia amri ya ulezi wa watoto wote wanne ambapo gharama za matunzo ya watoto hao zilipwe na Muombewa kila mwezi T.Shs. 250,000/= pamoja na gharama.

Katika kujibu Madai ya Muombaji, Muombewa amekubali ndoa yake na Muombaji itenguliwa na talaka itolewe, Nyumba na vitu vilivyotajwa na Muombaji pia amekubali viuzwe na kugawana nusu kwa nusu baina yake na Muombewa. Kuhusu watoto ameiomba Mahkama itoe amri ya kuwataka wabakie katika malezi yake kwani yeye ndiye anayegharamia mahitaji yao ya kila siku pamoja na masomo yao. Aliendelea kueleza kuwa watoto hao hivi sasa wanasoma Francis Maria Liberman School na pale anapoishi nao wameandaa usafiri wa kuwapeleka Skuli na kuwarudisha nyumbani.

Baada ya kupitia Hati ya Madai pamoja na ushahidi wa pande zote mbili katika shauri hili Mahkama hii inaona hoja pekee ambayo Muombaji na Muombewa wanapingana ni juu ya nani abaki na ulezi wa watoto. Mahkama hii inaona ni busara kwa watoto wawili wadogo wabaki katika usimamizi wa mama (Muombaji) ambapo Muombewa atatoa gharama za matunzo ya watoto hao. Kuhusiana na madai mengine ya kutenguliwa kwa ndoa na mgawanyo wa mali, Muombewa yote aliyakubali katika majibu yake ya madai. Hivyo basi Mahkama hii inatoa amri kama ifuatavyo:-

1. Ndoa, kati ya Muombaji na Muombewa inavunjwa na hivyo Muombaji na Muombewa si mke na mume tena.
2. Cheti cha Talaka kitolewe kwa Wadaawa.
3. Muombaji abaki na usimamizi na ulezi wa watoto Emmanuel Congress Mabengo na Stephen Congress Mabengo.
4. Muombewa abaki na usimamizi wa ulezi wa watoto John Congress Mabengo na Joyce Congress Mabengo.

5. Nyumba na vitu vyote vilivyotajwa na Muombaji viuzwe na pesa inayopatikana igaiwe nusu kwa nusu baina ya Muombaji na Muombewa.
6. Muombaji na Muombewa watakuwa na haki ya kuwaona watoto wakati wote kwa ruhusa ya msimamizi wa mtoto husika.
7. Kila upande ubege gharama zake.

Sgd: Rabia H. Mohamed

Judge

3/4/2013.

**AMRI:** Hukumu hii imesomwa leo taree 3 April, 2013 mbele ya Muombaji na Muombewa.

Sgd: Rabia H. Mohamed

Judge

3/4/2013.

***Nathibitisha kuwa hii ni Nakala halisi ya hati ya Asili.***

Sgd. **GEORGE J. KAZI**

MRAJIS

MAHKAMA KUU

**ZANZIBAR.**

